MAONI: Kuyatumikiza Mashamba ya Familia kwa Biashara na Vijana 'Wanabiashara –Kilimo'

Nteranya Sanginga ni Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki.

Nteranya Sanginga, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (International Institute of Tropical Agriculture - IITA). Picha ni kwa hisani ya IITA

IBADAN, Nigeria, Nov 23 2015 (IPS) – Kupata njia ya kuwaruhusu vijana kuchangia bidii na nguvu zao katika uzalishaji ndilo jambo kuu litakalochangia katika ufanisi na maendeleo ya bara la Afrika.

Ni kinaya kwamba vijana wa leo hata ingawa vijana hawa wanaunda kizazi ambacho kimesoma sana barani Afrika, hutatizika kujumuishwa katika maendeleo ya bara la Afrika.

Hali hii pia inapatikana katika mataifa yaliyoendelea. Lakini zaidi barani Afrika, ambapo asilimia sitini na saba ya idadi ya watu wake ambao hawana kazi ni vijana, idadi hii inakua kwa milioni 10 hadi milioni 12 kila mwaka. Changamoto hii inaendelea kukua. Leo hii kuna Waafrika milioni 365 walio kati ya umri wa miaka 15 hadi 35, na katika miaka 20 ijayo, idadi hii itakuwa mara mbili zaidi.

Hakuna njia nyingine. Ila tukubali kwamba vijana wenyewe ndio suluhisho.

Kila mtu mwingine- serikali, mashirika ya kimataifa, sekta ya kibinafsi, makundi ya kijamii na wazazi- wana jukumu kubwa katika ufanisi wa vijana na kwa hivyo watu hawa wasiwe vizuizi kwao. Mara nyingi, mtu husikia kuhusu haja ya kuchangia katika kubuni nadharia pana kutokana na haja ya kuwepo kwa ugawaji upya. Lakini ukweli ni kwamba, tunahitaji hatua za kimabadiliko kuhusu kilimo.

Hii ndiyo imani ya Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (International Institute of Tropical Agriculture - IITA) katika kutumikiza programu andalizi za '*uanabiashara-kilimo- (agripreneur)'.* Programu hizi zinalenga kutumia makundi ya kujiendeleza ili watu waweze kujisaidia. Kama nilivyoambia kundi la vijana nchini Uganda, tutatoa

msaada kwa njia ya teknolojia, maarifa na utetezi, lakini vitendo halisi lazima vifanywe nao. Ujumbe mwingine muhimu ni lazima wawe: “wakakamavu.”

Inajulikana vyema kwamba Afrika inayo ardhi ya kulima kubwa inayomilikiwa na wakulima wa familia, nyingi ya familia hizi huishi katika maeneo ya mashambani na mara nyingi hukumbana na njaa na umaskini. Takwimu zinaweza kuonyesha kwa urahisi jinsi mashamba mengi ya familia hutumiwa kama juhudi za kujikumu na mara nyingi kilimo chake hakifaulu bila msaada wa nje.

Kwa uhakika, ukulima wa familia ndio mkondo wa maisha. Lakini unapofikiria kwa kina, haimaanishi kwamba ukulima hauwezi kufanywa kama biashara. Wakati umefika wa kufanya kilimo kama biashara, hali hii inaweza kuwasilisha mabadaliko. Kufanya kilimo kama biashara kutaleta zana mpya za kuwavutia vijana wenye talanta katika sekta ambayo tunajua wazi kwamba wao huikwepa.

“Mamilionea na Mabilionea wa Afrika wa siku zijazo wataunda pesa zao kupitia kilimo.” Kama anavyopenda kusema Akinwumi Adesina, aliyekuwa waziri wa kilimo nchini Nigeria na sasa ni raisi wa Benki ya maendeleo ya Afrika (Africa Developmet Bank).

Na ni wazi kwamba vijana, ndio watasukumiza mabadaliko ambayo yatachangia katika kuboresha maisha badala ya kukimbilia mijini ambapo nafasi za ajira zinaendelea kupungua kadri idadi ya watu inavyoendelea kuongezeka. Zaidi, kilimo ndicho kimekuwa kiungo dhaifu katika uzalishaji wa ukuaji barani Afrika- hii ina maana kwamba kuna uwezo mkubwa wa kilimo kufanya vizuri kinyume na hali ya sasa.

Maarifa yanahitaji waenezi. Kwa kuwa huduma za kuwatembelea na kutoa maarifa kwa wakulima ni nzuri na zinahitaji kuboreshwa, vijana wana mbinu nzuri za kimawasiliano wakati wanapofikiria kwamba kitu ni kizuri na cha kufurahisha. Haya ndiyo yanayohitajika katika kilimo.

Kampeini ya Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (IITA) ya *uanabiashara-kilimo* (*agripreneur)* inategemea zaidi *mfano wetu wa maendeleo* ya Silicon Valley. Maeneo maalum yanaundwa ili kuruhusu vijana kujifunza na kubadilishana mawazo kwa njia halisi kuhusu jinsi ya uwajibikaji kifedha, mimea na mbinu mpya za ukulima, uwezo mkubwa wa thamani ya viungo vya kilimo ambavyo vinajumuisha majukumu ya wauzaji mbegu, wachataji chakula, watabiri wa hali ya anga, wauzaji wa bima, wataalamu wa mauzo..

Mmojawapo wa “wakufunzi” wetu wa uanabiashara-kilimo (*agripreneur)* aliniambia kwamba kile ambacho alijifunza ni kwamba ufanisi sio tu pesa. Biashara iliyowekezwa inahitaji mawazo, na uwezo wa kupanga mambo ipasavyo.

Kwa uwazi, msisimko wake- kama ilivyo na wanazuoni wetu- ni uwezo wa ujasiriamali. Unaojulikana kama uanabiashara kilimo. Waunganishi wa vifaa vya kilimo hutoa hili, ambalo hujumuisha mkururo wa fursa za ubadilishaji unaofanya kazi ili kuboresha utendakazi kwa wote na kuwatuza walio na talanta. Hiki ni kivutio kikubwa kwa vijana. Kimsingi, hali hii hufungua milango ya kukipa kilimo utaalamu.

Kwa uhakika, mfumo wa uanabiashara kilimo unahitaji hatua za ujumuishaji ili kuhakikisha kwamba mikopo inapatikana kwa vijana, hali hii itahakikisha kwamba usawa wa kijinsia unakuwa mojawapo ya misingi ya uendeshaji biashara wala sio lengo la kuafikiwa tu. Pia unahitaji mbinu nyinginezo kwa niaba ya kuimarisha umma ikiwa ni pamoja na utafiti wa kisayansi. Lakini hili linaanza na ubadilishaji wa mawazo kuhusu kilimo.

Watu lazima wajifunze kutuma maombi ya mkopo. Mara nyingi benki husema kwamba zipo tayari kuwafadhili watu kulingana na mpango wa biashara walio nao kuliko dhamana ya mkopo. Sasa ni wakati wa kutafuta mikopo kwa kutumia mipango ya biashara. Uzingatiaji wa Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki wa *uanabiashara- kilimo* ni msingi imara wenye mawazo kwamba hakuna anayejifunza kwa haraka isipokuwa vijana.

(Mwisho)